# Umuhimu wa Kazi ya Uchapishaji Leo

Na: Mch. Joseph Lusega | Mkurugenzi Idara ya Ucapishaji NETC

- Kazi ya kuwa mwanajeshi inahitaji moyo mkuu, inahitaji kujitoa, inahitaji ukakamavu na uvumilivu mkuu hiyo inatokana na mazingira ya kazzi yenyewe.
- Kwa ajili hiyo watu wengi wanaogopa kazi za jeshi kwa sababu ni ngumu,mazoezi yao ni magumu nk
- Ukweli ni kwamba kuwa mwanajeshi sio rahisi kunahitaji maamuzi ya dhati
- Hata hivyo wapo watu wajasiri, waliojitoa wakafundishwa hadi wakafauru
- Wakalipenda jeshi, kazi zake na mazoezi yake kuliko kitu kingine.
- Kama ungepata fursa ya kuhoji mmoja mmoja wangekupa ushuhuda jinsi walivyoingia katika kazi hiyo.
- Huenda wengine wangekueleza kuwa waliingia jeshi kwa sababu walizaliwa na kuishi mazingira hayo na hivyo wameyazoea
- Wengine wangekuambia waliingia jeshi kwa hiari bila kujali ugumu wake, amani na ulinzi wa uhuru wanchi yao lilikuwa kusudi kubwa kwao
- Lakini wapo wanajeshi walioingia humo kwa faida zao binafsi hao ndio hawana mwelekeo na umoja kamili na wenzao-ugumu wa kazi ukizidi hutoroka jeshi na kuacha
- Ndio maana katika nchi zingine jeshini kunakuwa na uasi ugomaji hata kufanya mapinduzi ya kijeshi.

Watendakazi katika taasisi zetu na washiriki wote wa kanisa ni wanajeshi wa Bwana walio katika vikosi mbalimbali vya mapambano ya wema na uovu. Hii ni vita baina ya Kristo na Shetani

- Kila muumini wa Kiadventista wa sabato ni askari vitani bila kujali uliingiaje humu
- Tendo la kumpokea Kristo linakuwajibisha kazi ya uaskari wa Kristo
- Agizo la Jemedari Yesu Waefeso 6:11

Jeshini kuna vikosi mbalimbali kwa mfano

- Vikosi vya mstuni
- Vikosi vya nchi kavu
- Vikosi vya baharini
- Vikosi vya anga na mizinga

Vivyo hivyo na kanisani tuna vikosi mithili ya jeshini navyo ni;

- Idara ya shule ya sabato
- Idara ya Vijana
- Idara ya Wanawake
- Adventist Men/Dorcas na nk.

Vikosi hivi viko kwa kila Kanisa,lakini jambo la kusikisha ni kwamba kikosi cha anga na mizinga hawapo kwa kila kanisa ni makanisa machache au mitaa michache iliyo na kikosi hiki (kikosi hiki kwa kanisani nimekifananisha na w/v) na wakuu wa vituo vyetu hawashituki

Uinjilisti wa vitabu ni kikosi cha anga na mizinga ukweli ndio kiini cha mashambulizi ya vita hii isiyoonekana kwa macho ya kibinadamu hadi mwisho wa wakati

Ndiyo maana kuna pendekezo la ulimwengu mzima kuwarudisha waumini wote na kuwaingiza wote katika kikosi hiki cha anga na mizinga ndilo kusudi hasa la wito wa washiriki kutawanya kwa watu Tumaini kuu/Afya na uzima na machapisho mengine.

- Kwa kweli ingependeza kama kila kanisa lingekuwa angalau 1- 3
- Lakini roho ya unabii inasema palipo na m/v mmoja wanatakiwa mia moja
- Sehemu zingine zinasema washiriki wetu wote wanatakiwa kutoka na kutawanya vitabu na magazeti yetu **Kutayarisha Njia 1 uk.82,67**
- Waefeso 6:11 Mwanajeshi unatakiwa kuvaa silaha zote za Mungu (mbinu zote)

**Umuhimu wa kazi ya uchapishaji leo**

- Hii ndiyo idara iliyoandikwa kwa roho ya unabii kuwa itatenda kazi na kuimaliza hata mwisho
- Hebu fikiri dunia bila vitabu vya neno la Mungu ingekuwaje, ni sawa na dunia bila jua
- Kanisani kwetu ukiondoa vitabu vya roho ya unabii hatutakuwa na tofauti yoyote na watu wa madhehebu mengine

**Biblia imeandikwa na watu wa aina mbalimbali**

- Wasomi na wasio wasomi
- Wenye cheo na wasio na cheo
- Wakulima na wafanya biashara
- Lakini maandiko yao yanapatana japo waliandika watu tofauti na nyakati tofautitofauti
- Roho wa Mungu ndiye wavuvia na aliyewaongoza
- Kazi ya Mungu itafanywa na makundi ya aina zote maana kiongozi ni Roho Mtakatifu

**Kazi ya uinjilisti wa vitabu ilianzishwa na Mungu mwenyewe**

1. Kwa makusudi ya kulea watu wke kiroho
2. Na kuendeleza kazi ya utume mbele na kuimaliza

   Kwa hiyo uinjilisti wa vitabu unaongoa roho,unalea washiriki na kutunza kiroho.

Kwa nini makanisa mengi katika mitaa mingine hayana w/v wa kutosha?

- Watu wanaogopa ugumu wa kazi yenyewe
- Wengi wanapenda kazi rahisi wanaangalia faida ya dunia hii tu
- Roho ya unabii inasema kazi hii ilianza kwa kujinyima na itamalizika kwa kujinyima **eleza kusimika kazi ya Mungu kipindi cha akina James White**
- **Soma His Massenger pp, 89,95**

**Daniel 9:1-2**

- Danieli alifahamu mambo kwa kusoma vitabu- kwa kusoma vitabu tutafahamu dalili na nyakati za kurudi kwa Yesu
- Ukiwahubiri watu bila kuwapa vitabu watasahau haraka – lakini wape watu vitabu watakumbuka
- Uamusho na matengenezo hauji watu wasiporejea katika usomaji wa neno Biblia na roho ya unabii
- Katika siku za akina Martin Luther uamusho na matengenezo ulikuja kwa kuvisoma vitabu – Biblia ilisomwa kwa dhati
- Aligundua makosa 95, alitafsiri Biblia katika lugha ya kijerumani
- Mitume kwa miaka 3 ½ waliandika, ili neno alilosema Yesu lidumu milele
- Paulo aliagiza vitabu vyake vya ngozi toka troa
- Wakati Mungu alipowakomboa wana wa Israel toka Misri akiwarudisha watu wake katika ibada halisi pale Sinnai Mungu alianza na idara ya uchungaji na uchapishaji **Kutoka 31:18** inakadiriwa kwenye miaka **1500 BC**
- Siku za Ellen White mwanaume mmoja Hazenfoss alipewa na malaika ujumbe huu ili aandike njozi akakataa mama White akakubali miaka 1848 AD zaidi ya miaka 4000 Mungu ameliongoza Kanisa lake kwa idara hizi.

Wapendwa vitabu vya waandishi wa dunia hii vya mwaka 1844 AD havipo hata nukuu zao hazipo – na hata zingekuwepo huwezi kuzifanyia rejea (reference)

- Wahadhili (Lectures) wasingekukubalia ufanyie research Paper vitabu hivyo
- Lakini vitabu vya mama White vilivyoandikwa mwaka 1848 vinasimama hadi leo kadri mwisho unavyokaribia ndipo vinazidi kuwa soko (thamani) duniani.
- Ndani ya kanisa wachache watapinga mpango huu wa Mungu haijalishi wawe wachungaji wazee wa kanisa au washiriki tu wa kawaida lakini ukweli utashinda tu maana umenenwa na asiyekosea.
- Mungu anahitaji tushirikiane katika idara zote ili tumalize kazi tusibague wala kupendelea idara fulani fulani tu, kumbuka agizo la Yesu vaa silaha zote za Mungu tupate kuyapinga majeshi ya shetani

**Namna ya kushiriki jitoe**

- Kufanya juma la watendakazi (Big week)
- Fanya kazi kama F/T, P/T au kama manafunzi student programe
- Kwa shiriki kugawa kitabu cha mwaka na machapisho mengine uinjilisti wa washiriki
- Unapojiandaa kutumika kupitia machapisho endelea kuwaombee w/v

Katika mianzo ya kazi yetu ya uchapishaji,nabii alisema kwamba washiriki wa kanisa WAUZE au WAGAWE BURE vitabu na magazeti(Angalia Manuscript 126, 1902).

Ellen G. White Anasema; "Hilo ndilo Mungu analolitaka kanisa lote lijihusishe katika kuyafikia na ujumbe makundi yote ya watu" (angalia *Review and Herald*, January 17, 1893).

"Kila muumini (SDA)anaitwa kusambaza karibu na mbali vijizuu magazeti na vitabu vyenye ujumbe wa wakati huu." (Review *and Herald*, November 5, 1914)